# CENTRAL ZONAL EXAM

**KISWAHILI
SEHEMU YA
KWANZA:
LUGHA**

## DARASA LA SABA
## MUHULA WA TATU -

***JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU*** **Muda: Saa 1 Dakika 40**

1. *Tumia penseli ya kawaida.*
2. *Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:*
   *(I) NAMBARI YAKO YA MTIHANI (II) JINA LAKO (II) JINA LA SHULE YAKO*
3. *Kwa kila swali onyesha jibu sahihi kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndiyo jibu.*

---

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1-15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Siku saba __1__ tangu mwana wangu mpenzi __2__. Jioni __3__ nilikuwa __4__ huko na huko chumbani __5__ nikifikiri, __6__ nilisikia mlango __7__. Nikaenda __8__ mlango __9__. Lo, nilipotazama kumbe __10__ zangu __11__ zamani Abdi Nzuma, Yusuf Kipanga, Petero Mwongozo, Zainabu Karata na Bahati Sudi __12__ nje. Niliwasalimia lakini __13__. Walinikabidhi __14__ kwa unyenyekevu kisha wakaenda __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. zimepita | B. imepita | C. yamepita | D. kumepita |
| 2. | A. alizikwa | B. alipogonjeka | C. amelala | D. alipougua |
| 3. | A. ilipokuja | B. ilipofuata | C. ilipofika | D. ilipokuwa |
| 4. | A. nitatembea | B. ninatembea | C. nikitembea | D. nitembee |
| 5. | A. mwangu | B. changu | C. yangu | D. wangu |
| 6. | A. wakati | B. kama | C. mara | D. muda |
| 7. | A. ukipigwa | B. ukibishwa | C. unabishwa | D. ukipishwa |
| 8. | A. kuufunga | B. kuifungua | C. kufungua | D. kuufungua |
| 9. | A. yenyewe | B. penyewe | C. mwenyewe | D. wenyewe |
| 10. | A. marafiki | B. rafiki | C. warafiki | D. wapenzi |
| 11. | A. wa | B. ya | C. za | D. waliko |
| 12. | A. wapo | B. walikuwa | C. wamo | D. waliko |
| 13. | A. hawakujibu | B. waliitikia | C. walijibu | D. hakuitika |
| 14. | A. madawa yao | B. dawa yao | C. madawa zao | D. dawa zao |
| 15. | A. makwao | B. nao | C. zao | D. kwao |

***Kutoka swali la 16-30 chagua jibu lililo sahihi.***

16. Kanusha: Nimekunywa ________
A Sijanywa B. Sijakunywa
C. Sitakunywa D. Sinywi

17. Neno "wadhifa" liko katika ngeli gani?
A. A-WA B. U-U
C. U-ZI D. I-ZI

18. Mtoto mgonjwa ni __________ kiashiria kisisitizi ni kipi?
A. uu huu B. huyu huyu
C. yuyu huyu D. yuyu huyo

19. ***Kamilisha methali:***
"Meno ya mbwa ____________"
A. hayaumi B. hayavunjiki
C. hayaumwi D. hayaumani

20. Mjomba alipigwa kalamu. Maana ya nahau hii ni:-
A. alipandishwa cheo kazini
B. alipigwa sana
C. aliachishwa kazi
D. alistaafu

21. ***Andika katika usemi halisi.***
Mwalimu alimwita Ali aende alipokuwa.
A. "Njoo hapa", Mwalimu alimwita Ali.
B. "Njoo hapa nilipo," mwalimu alimwita Ali.
C. "Njooni hapa." Mwalimu alimwita Ali.
D. "Njoo," mwalimu alimwita Ali.

22. "Shamba lake ni bahari" ni tamathali ya lugha inayoitwa____
A. tashdidi B. tashbihi C. nahau D. istiara

23. Chagua sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.
A. Shuleni tunasoma masomo yafuatayo; Kiswahili, Hisabati, Kiingereza, Sayansi, Elimu jamii na Dini
B. Shuleni tunasoma masomo yafuatayo: Kiswahili, Hisabati, Kiingereza, Sayansi, Elimu jamii na Dini
C. Shuleni tunasoma masomo yafuatayo Kiswahili, Hisabati, Kiingereza, Sayansi, Elimu jamii na Dini
D. Shuleni tunasoma masomo yafuatayo: Kiswahili, Hisabati, Kiingereza Sayansi, Elimu jamii, Dini.

24. Chagua sentensi iliyotumia kirejeshi -amba kwa usahihi.
A. Mti ambao unaokatika ni huu
B. Mti ambao ukatikao ni huu
C. Mti ambayo unakatika ni hii
D. Mti ambao unakatika ni huu

25. Mavyaa na bavyaa ni wazazi wa ________
A. mke B. mume
C. shangazi D. binamu

26. Ni ipi si maana ya neno "kuna"
A. Kuambua magamba ya samaki
B. Kutumia mbuzi kusugua nazi
C. Kuwako, kuwa huku na huko
D. Kusugua panapowasha

27. ***Chagua kiunganishi sahihi kujazia pengo.***
Shule yetu ina kila kitu ________ tarakilishi.
A. ilhali
B. ijapokuwa
C. ila
D. ingawa

28. Eleza matumizi ya kwa katika sentensi ifuatayo.
Alienda Ughaibuni kwa meli.
A. kuonyesha mahali
B. kuonyesha uhusiano
C. kuonyesha sababu
D. kuonyesha matumizi

29. Myunani ni mwananchi wa nchi ya ________
A. Ureno B. Uturuki
C. Ugiriki D. Unguja

30. Kivumishi cha sifa kutokana na kitenzi iva ni:-
A. mbivu B. ivisha C. ivisha D. mbifu

***Soma kifungu kifuatacho, kisha ujibu maswali 31-40.***

**Chama cha Kiswahili,**
**Shule ya msingi ya Hekima,**
**S.L.P 1012,**
**KINANGOP**
**20/9/2013**

**Mkurugenzi mkuu,**
**Kituo cha Habari na utangazaji,**
**S.L.P 1234,**
**NAIROBI.**

**Bi. Mkurugenzi.**
**MINT: SHUKRANI**

Chama cha Kiswahili shuleni mwetu kingependa kukushukuru kwa kuturuhusu kutembelea kituo chako cha habari na utangazaji.

Tulifurahi kuona vile waandishi wa habari hukusanya habari wakitumia kanda za kunasia sauti za video pamoja na mtandao wa mawasiliano. Tulishuhudia vile wao huziwasilisha katika chumba cha habari kwa nj a mbalimbali za

mawasiliano kama vile simu za kawaida, rununu au simu tamba, kipepesi na bama pepe. Aidha tulishukuru kuona vile habari hutayarishwa kwa matumizi ya tarakilishi kabla ya kuandikwa kwenye magazeti au kupeperushwa hewani kwa usaidizi wa satilaiti ili zifikie hadhara.

Tuliduwaa waa kuona kuwa habari pamoja na takwimu nyingine huhifadhiwa kwenye ngamizi zizo hizo kwa marejeleo ya baadaye. Kitu kingine kilichotuvutia ni vipasa sauti ambavyo si vikuba kama vile tulivyozoea.

Yakini, kutembea kwingi kuona mengi. Halikadhalika, jambo lililotusisimua kabisa ni kuona vile vipindi nui vya watoto hutayarishwa ili visikike kwenye redio au vionekane kwenye runinga.

Jambo hili lilitutia shaulu ya kushiriki katika vipindi kama hivyo na hivi karibuni twatumaini kuandika waraka kukuomba utupe fulsa ya kushiriki katika kipindi kimojawapo. "Mchovya asali hachovyi mara moja" - ndivyo wasema wanachama huku wakizidi kukushukuru.

**Wako mwaminifu,**

**Utu Bora.**
**Katibu Mkuu.**

31. Barua rasmi ina anwani ngapi?
A. Tandatu
B. Thenini
C. Aroba
D. Mosi

32. Ni chama gani kilitembelea kituo cha habari na utangazaji?
A. Chama cha mkurugenzi mkuu
B. Cham cha habari na utangazaji
C. Chama cha Kiswahili
D. Chama cha Utu Bora

33. Waandishi wa habari hukusanya habari wakitumia nini?
A. Kanda za kunasia sauti, video, mtandao wa mawasiliano
B. Kanda za kunasia sauti, magazeti, rununu
C. Video, mtandao wa mawasiliano, tarakilishi
D. Tarakilishi, sitilaiti, barua pepe

34. Barua hii ilikuwa inaandikiwa nani?
A. Utu Bora
B. Chama cha Kiswahili
C. Kituo cha habari
D. Mkurugenzi mkuu

35. Chama hiki kilishuhudia kuona vile habari huwasilishwa katika chumba cha habari kwa njia mbalimbali za mawasiliano kama vile:-
A. satilaiti na ngamizi
B. magazeti na simu tamba
C. kipepesi na barua pepe
D. video na mtandao

36. ________ hutumiwa kama njia mojawapo ya teknolojia ya kutayarisha habari.
A. tarakilishi
B. magazeti
C. barua pepe
D. video

37. Habari na takwimu nyingine huhifadhiwa kwenye sehemu ya ________ kwa marejeleo ya baadaye.
A. vipasa sauti
B. satilaiti
C. kompyuta
D. rununu

38. Neno jingine lenye maana sawa na runinga ni:-
A. ruyoga
B. ngamizi
C. kipakatarishi
D. televisheni

39. Jambo lililowasisimua zaidi wanachama ni?
A. Namna habari hupeperushwa hewani kwa usaidizi wa satilaiti
B. Namna habari huwasilishwa katika chumba cha habari
C. Jinsi vipindi mbalimbali vya watoto hutayarishwa ili visikike kwenye redio au vionekane kwenye runinga
D. Jinsi ya kushiriki katika vipindi vya redio na televisheni kwani mchovya asali hachovyi mara moja

40. Chagua sehemu tano muhimu za barua rasmi.
A. Anwani, tarehe, salamu, utangulizi, wasalaam
B. Anwani, tarehe, utangulizi, mada, wasalaam
C. Anwani, tarehe, salamu, fani za lugha, mada
D. Anwani, tarehe, utangulizi, mada, fani za lugha

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.***

Tayari takribani miongo ya miaka imepita tangu tujinyakulie uhuru kutoka kwa wabeberu. Wakoloni walipofunganya virago na kujiendea zao, sisi Wafrika tulichukua hatamu. Madhumuni yaliwekwa na mikakati ya kufuatwa ikatayarishwa.

Azma zilizopewa kipaumbele ni kuuzika ujinga na upuuzaji, kuangamiza uchochole na maradhi kwa kuwapa raia wetu mahitaji ya kimsingi. Maneno kama vile "maji kwa wote kufikia .........." yalisikika kila uchao. Watawala kwa watawaliwa wakawa na matumaini makuu. Lakini leo hii mambo ni tofauti. Ijapokuwa kama nchi tumepiga hatua kadha wa kadha katika nyanja mbalimbali, bado malengo yetu ya wakati wa uhuru hayajatimia.

Taratibu, mambo yalianza kwenda upogo. Meli yetu ikaanza kuyumbayumba. Matumaini ya wazalendo ya kufikia ng'ambo ya pili - ng'ambo ya ustawi na ustaarabu yakaanza kudumaa. Nafasi ya uzalendo ilichukuliwa na ubinafsi. Abiria wa meli wakaanza kuzozana. Wengi wakaugua kansa ya ukabila. Ni dhahiri shahiri utengano uondokapo hupisha udororaji na balaa tele.

Tamati ya yote hayo, mambo yamezidi kutokota. Ufukara umekita mizizi. Zaidi ya asilimia sitini ya wananchi wanaishi katika kitovu cha uchochole, umaskini wa kupindukia. Maji safi na salama ni neno geni kwa wengi nchini. Wengi wanazidi kusumbuliwa na maradhi kama vile homa ya matumbo na waba. Ajira nayo inazidi kuwa nadra. Vijana tele wanazidi kukanyaga lami licha ya kuwa na vyeti vya elimu na hata taaluma mbalimbali. Hatuna budi kupiga darubini kama taifa tuone ni wapi tulipoteza shabaha. Kisha tupige msasa. Ukweli ni kuwa tunao uwezo wa kupiga hatua mbele. Mradi tu tushirikiane. Tuelewe kuwa malengo yakiwa pamoja, kilicho mbali huja karibu.

**41.** Ni yapi yaliyotokea pindi wakoloni walipoondoka nchini?
A. Uhuru ulipatikana
B. Raia walipata mahitaji ya kimsingi
C. Malengo yalipewa kipaumbele
D. Mbinu za kufikia ufanisi zaidi ziliwekwa

**42.** Orodha ganu inaonyesha mahitaji ya kimsingi pekee?
A. Ushirikiano, makazi, elimu, chakula
B. Matibabu, makazi,lishe, elimu
C. Matibabu, makazi, madaraka, chakula
D. Makazi, uongozi, elimu, chakula

**43.** Mwandishi anasema:-
A. Taifa letu halijabaki nyuma kimaendeleo
B. Nchi yetu haijapata maendeleo yoyote
C. Nchi yetu haijapata maji safi
D. Taifa letu halijatimiza malengo mengi ya tangu hapo awali

**44.** Ni lini mambo yalianza kwenda mrama?
A. Ibinafsi wa meli ulipoanza kuyumbayumba
B. Ubinafsi na maovu mengine yalipowakumba raia
C. pindi tu waafrika walipochukua usukani wa uongozi
D. Mara tu mzungu alipotukabidhi uhuru wetu

**45.** Kulingana na habari, <u>**abiria wa meli**</u> ni kina nani?
A. Viongozi
B. Mabeberu
C. Maskini
D. Raia

**46.** Nafasi ya uzalendo ilichukuliwa na ubinafsi. Ni nini maana ya kifungu hiki?
A. Watu walianza kupendana wao kwa wao
B. Watu waliacha kufikiria matakwa ya taifa na badala yake wakajifikiria zaidi
C. Wazalendo walikuwa watu binafsi
D. Watu walianza kupendana na kushirikiana katika ujenzi wa taifa

**47.** Ndwele ya homa ya matumbo husababishwa na:-
A. utumiaji wa maji na chakula kisicho salama
B. ukosefu wa lishe bora
C. kupumua hewa chafu
D. vidudu viishivyo katika maji yaliyotuwama

**48.** Ukosefu wa utengamano husababisha:-
A. saratani
B. ufanisi
C. umaskini
D. ukoloni

**49.** Mwandishi anatoa pendekezo lipi kwa masaibu yetu?
A. Tuishi kwa imani
B. Tuondolee mbali ubinafsi
C. Tuwe na nia moja tu
D. Tujikinge kutokana na maradhi

**50.** Chagua jibu lililo sahihi kulingana na taarifa hii.
A. watu wengi wanaugua saratani
B. mwandishi haoni matumaini yoyote kufikia malengo yetu
C. wakoloni wanastahili kulaumiwa kwa janga zetu
D. mwandishi ni mzalendo kamili